KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 22, Issue 1

13th Jumaadal Aakhira 1433

4th MAY, 2012

WALIOFILIWA KUWATAYARISHIA WATU CHAKULA

Abu Bakr al-Turtushi al-Maliki (k. 520H) ameandika: Wanavyuoni wetu wa ki-Maaliki wamesema: Kuweka maandalizi ya tanzia (mipangilio ya vikao) ni jambo la Uzushi na la kuchukiza. Kwahiyo, [aliyefikwa na msiba wa kifo cha mtu wake] na akae nyumbani mwake, au msikitini, akiwa katika hali ya kuhuzunika, lakini na asijiweke kama anaengojea kupokea tanzia. Katika hali kama hii hapana ubaya wowote. Pindi habari za kifo cha Ja'far zilipomfikia Mtume (صلى الله عليه وسلم), alikaa msikitini, huzuni zikamjaa tele na watu wakaanza kumtazii. Amesema Maalik, hapana ubaya iwapo waliofiwa watapelekewa chakula, pasi na kujali iwapo jamaa wa kumuhusu au laa. Na hii ni kwa sababu amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم), zilipotujia habari za kifo cha Ja'far [bin Abi Talib], *'Watayarishieni chakula jamaa za Ja'far, kwani wamepatwa na yenye kuwashughulisha wao.'*

Na chakula hichi kimependekezwa kwa rai ya kundi la wanavyuoni, kwa sababu ni kutokamana na (amali za) wema na mkuruba kwa jamii na majirani wote, na kwahivyo imependekezwa (mustahabb). Lakini ikiwa jamii (ya waliofiwa) itawatayarishia watu chakula na kuanza kuwakaribisha waje wale, hakuna chochote kilichopokewa kuhusiana na hayo kutoka kwa watu wema waliotutangulia (Qudumaa), na kwa maoni yangu, hayo ni mambo ya uzushi yenye kuchukiza. Na rai hii imetokana na yale ambayo ash-Shaafi'ee ameyakubali. **Al-Hawadith wal-Bida' (Dar Ibn al-Jawzee, Uk. 170-171)**

Shaykh Abd al-Aziz bin Baz (رحمه الله) amesema: "Ama kwa jamii ya waliofiwa kutayarisha chakula na kuwaalika majirani (waje wale chakula hicho), basi jambo hilo si sawa, bali ni katika mambo ya uzushi, na katika madhambi maovu. Jarir bin Abdullah al-Bajli (رضي الله عنه) amesema: "Tulikuwa tukichukulia kukusanyika pamoja na jamii ya waliofiwa na kutayarisha chakula baada ya mazishi ni katika *niyahah* (sampuli iliyokatazwa ya maombolezi inayotokamana na zama za ujinga). Jarir (رضي الله عنه) alitueleza yakwamba walikuwa wakichukulia vile watu wanavyokusanyika pamoja na jamii ya waliofiwa na kutayarisha chakula kwa watu, yakwamba haya yalikuwa ni katika niyahah, kwa maana yakwamba Maswahaba walikuwa wakiyazingatia hayo kuwa ni miongoni mwa hayo. Hii yaonyesha yakwamba jamii ya waliofiwa haifai kuwatayarishia watu chakula, na wala wasiwakusanye pamoja. Ingawaje, imependekezwa kwa majirani zao na jamaa zao wawapelekee [wao waliofiwa] chakula kwa vile wao wameshughulishwa na mkasa huo wa kifo.

Fatawa Nur ala al-Darb (1/369) kupitia al-Bida' wal-Muhdathaat (p. 336).

Shaykh al-Albani (رحمه الله) amesema: "... Hii imetokana na hadeeth ya Jarir bin Abdullah al-Bajli (رضي الله عنه) aliesema: "Tulikuwa tukichukulia kule kukusanyika na jamii ya waliofiwa na kutayarisha chakula baada ya mazishi ni katika niyahah (sampuli iliyokatazwa ya maombolezi inayotokamana na zama za ujinga). Sunnah ni kwamba watu wa Yule aliyekufa na majirani na wawatayarishie chakula jamaa za aliyekufa kitakachowatosha wao, kutokana na hadeeth ya Abdullaah bin Ja'far (رضي الله عنه) aliesema: "Tulipojiliwa na habari ya kifo cha Ja'far, alipouwawa, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema, watayarishieni jamaa za Ja'far chakula, kwa sababu wamejiliwa na mambo yaliyowashughulisha wao …" na hadeeth ni hasan. **Ahkaam al-Janaa'iz (p. 167).**

Shaykh Salih al-Fawzan amesema: Kutoka pole anapokufa mtu ni jambo la ki-sheriya kwa sababu ni katika pembe ya kuwafariji au kuwaliwaza, na vilevile imehusisha du'aa' kwa aliyekufa. Hii ni kwa Yule mwenye kutoa pole atakapomwambia aliyefiliwa na jamaa yake, "Namuomba Allaah akufariji, akusahilishie mkasa ulokufika na amsamehe aliyekufia." na haipendekezi pale kuwe na nyongeza katika kuwafariji waliofiwa, kama vile kutengeneza mahema, na kukusanya watu wengi na kutochunga mipaka katika kutayarisha vyakula na makaramu. Jarir bin Abdullah al-Bajli (رضي الله عنه) amesema: "Tulikuwa tukichukulia kukusanyika pamoja na jamii ya waliofiwa na kutayarisha chakula baada ya mazishi ni katika *niyahah* (sampuli iliyokatazwa ya maombolezi inayotokamana na zama za ujinga). Sunnah ni kwa mmojawapo wa jamaa zake au majirani zake, watayarishe chakula kulingana na mahitaji na awapelekee. Hii ni kutokana na hadeeth ya Abdullaah bin Ja'far (رضي الله عنه) aliesema: "Tulipojiliwa na habari ya kifo cha Ja'far, alipouwawa, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema, watayarishieni jamaa za Ja'far chakula kwa sababu wamejiliwa na mambo yaliyowashughulisha wao …" au "… lenye kuwashughulisha wao limeshawajia." Na haifai kutenga mahali maalum kwa kupokea pole na kutangaza. Lakini aliyefikwa na msiba huo anaweza kupewa pole mahali popote aonekanapo, na inatakiwa isiwe umepita muda mrefu baada ya kifo hicho. Na Allaah Ndiye Mjuzi zaidi." **Al-Muntaqaa (1/196-197).**

Si katika Sunnah, kutokana na yaliyotangulia kwa jamaa za waliofiliwa kujitolea na kufanya maandalizi ya kupokea pole kwa

YALIYOMO

CHAKULA CHA MAITI 1

MIUJIZA YA MTUME 2 - 4

USIKOSE MAWAIDHA YA KUHUSU TAWHEED KATIKA MSIKITI WA MAZ-RUI KILA SIKU BAADA YA MAGHRIB MPAKA 'ISHAA'. NA USTADH NA'MAN

kuandaa na kutayarisha vikao maalum vya kupokea pole hizo. Ama kuwapokea na kuwakaribisha waliokuja kuwapa pole kama sehemu tu ya matukio ya kawaida ya kilimwengu (kwa vile hai-epukiki kwa jamaa za waliofiwa kufanyiwa ziyara za majirani na jamaa zao).

SUALI: Ni nini rai yako kumuhusu mwenye kukaa nyumbani kwake akiwapokea wenye kuja kumtazii (kumpa pole), licha ya kujua kwake yakwamba watu wengi wenye kuja kutoa pole hizo hawawezi kufanya hivyo isipokuwa kwa kuja nyumbani kwa aliyefiwa?

JAWABU: Mimi sioni ubaya wowote kumuhusu aliyefikwa na msiba kama vile kifo cha jamaa aliyemuhusu, au mkewe na yanayofanana na hayo kwake yeye kuwapokea wenye kuja kumtazii nyumbani kwake katika wakati maalum, kwa sababu ta'ziyah (kutoa pole) ni Sunnah na kuwapokea wenye kuja kutoa pole ni kutokamana na yenye kuwasaidia wao katika kuitekeleza Sunnah hiyo. Na lau kama angeliwakaribisha Chai au kahawa, au hata manukato, basi yote hayo ni mambo mazuri. **Majmu' Fatawa of Ibn Baz (13/384).** Ama kuhusu mas'ala iwapo jamaa za waliofiwa wanaweza kushirikiana katika kula chakula walichotayarishiwa wao na watu wengine wakawaalika kula nao.

SUALI: Jamaa za waliofiliwa wanapopelekewa chakula cha mchana au cha usiku, na watu wengine nao wakajumuika kula pamoja nao katika nyumba ya waliofiliwa, jee [chakula] hicho pia huzingatiwa kuwa miongoni mwa chakula kilichokatazwa cha niyaahah? **JAWABU:** Laa, hiyo si katika niyaahah (maombolezi ya haram), kwa sababu wao hawakutayarisha chakula, lakini walitayarishiwa. Na hapana makosa ikiwa watawakaribisha watu wengine wale nao kwa sababu huwenda chakula chenyewe kikawa kingi hata kuliko wanavyohitaji. **Majmu' Fatawa of Ibn Baz (13/398).**

Fatwa hii inataka ieleweke juu ya muangaza wa yaliyotangulia yakwamba si juu ya jamaa za waliofiwa kufanya tasaddee (kujitweka) kwa kupokea ta'ziyah kama ilivyo, kutoka nje na kuwapokea watu wanaokuja kuwatazii, kwa kutayarisha vikao makhsusi, na wala jamaa wale wasilipe pesa kwa ajili ya kupikwa na wengine kwa malengo ya kuwalisha watakaokuja na kukusanyika nyumbani kwao, kwa sababu hilo litawarudia jamaa waliofiwa wenyewe wachukuwe majukumu ya mapishi (hata kama si wao waliopika kwa nguvu zao) na kujitweka uzito, na hili litarudi kwenye niyaahah iliyoharamishwa (maombolezi) yaliyotajwa na Jarir bin Abdullah al-Bajli (رضي الله عنه).

MIUJIZA YA MTUME MUHAMMAD (صلى الله عليه وسلم) [Prt 2]

[Endelea Kutoka Vol. 87, Issue 2]

Mtume (صلى الله عليه وسلم) kisha akasoma, "Hakika Sisi Tulikwishampa Musa Kitabu". Hivyo usiwe na mashaka juu ya kukutana na Musa (عليه السلام) huko mbinguni katika usiku wa Mi'iraaj (Al-Bukhaariy Juzuu 4 Namba 462].

Na kwa riwaya nyingine, Anas bin Maalik amesema, "RasuluLlaah (صلى الله عليه وسلم) alisema, "Katika usiku wa Mi'iraaj nilipopandishwa kupelekwa Mbinguni nilipita karibu na watu ambao walikuwa wana makucha ya shaba na walikuwa wakijiparura nyuso zao na vifua vyao. Nilisema; Hawa ni nani ewe Jibriyl? Alijibu na kusema kuwa: Hawa ni wale watu waliokuwa na tabia ya kusengenya na kuwazulia watu maneno machafu na kuharibu heshima za watu" [Sunan Abu Daawuud namba 4860]. Na katika riwaya nyingine, Abu Hurayrah anasema: RasuluLlah alisema: "Katika usiku wa Mi'iraaj nilipopelekwa Mbinguni niliona watu ambao matumbo yao yalikuwa makubwa kama nyumba na ndani yake kuna majoka ambayo yalionekana nje ya matumbo yao. Niliuliza kuwa walikuwa kina nani, na Jibriyl alinijibu kuwa wao walikuwa wale watu waliokuwa wakila mali ya riba". [Musnad Ahmad, Ibn Maajah na At-Tirmidhiy namba 2828]. Kasema Anas bin Maalik (رضي الله عنه): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema, "Usiku wa Mi'iraaj nilipopelekwa Mbinguni niliwakuta watu na midomo yao ikichanwa na mikasi ya moto. Nikamuliza Jibriyl ni nani hao na akasema walikuwa ni wahubiri miongoni mwa wafuasi wangu, ambao walisema ambayo wao hawakuyafanya" [At-Tirmidhiy (ghariyb) Namba 4801]. Buraydah bin Al-Haasib (رضي الله عنه) alieleza jinsi siku moja asubuhi Mtume (صلى الله عليه وسلم) alivyomwita Bilaal na kusema, "Umefanya nini mpaka ukaingia Peponi kabla yangu? Sikupata kuingia peponi pasina kusikia mchakacho wako ukiwa mbele yangu. Bilaal akajibu, 'Sijapata kuadhini ila baada yake kuswali rakaa mbili. Na sijapata kutenguka wudhuu ila nilitawadha papo hapo na kujiona kuwa nina deni kwa Allaahla rakaa mbili. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema, "Ni kwa sababu hizo," [At-Tirmidhiy namba 326]. Na Jaabir bin 'Abdullaah (رضي الله عنه) alisema: Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema, "Nilijiona naingia Peponi na mara nikamwona bi Ar-Rumayswah, mke wa Abu Twalhah. Nilisikia hatua za mtu. Nikauliza, "Wewe nani?". Mtu mmoja akajibu: "Ni Bilaal" kisha nikaona kasri na mwanamke akiwa amekaa katika ukumbi wake. Nikauliza, "Kasri la nani hili?" Basi kuna mtu alijibu, "Hilo la 'Umar" Nikatamani kuingia ili nione ndani kukoje, lakini nilikumbuka jinsi 'Umar alivyo na wivu (ghiyrah) basi sikuingia" Mara 'Umar akadakiza "Fidaka Abiy wa Umiy, Yaa RasulaLlaah! Nitathubutu namna gani mimi kudhania kuwa umenikosea wewe kwa kuingia kwangu?" [Al-Bukhaariy Juzuu 5 Namba 28].

Kutokana na Hadeeth hizi tunaona jinsi Mtume (صلى الله عليه وسلم) alivyokuwa mtu mwenye kulea watu wake na kuwafundisha mambo kwa hekima. Alipowafundisha tabia njema haikuishia bali yeye aliyafanya hayo kwa mifano ya wazi wazi kabisa. Alipata kusema, "Kama mtu atachungulia katika nyumba ya mtu bila rukhsa ya mwenyewe na huyo mwenye nyumba akachokora jicho lake, kutakuwa hakuna tatizo wala hilo jicho halitalipwa fidia". [Sunan Abu Daawuud namba 5153]. Kwa sababu yule anayechungulia katika nyumba za watu amefanya wizi kwa kuingilia siri za watu na hifadhi zao na hivyo Allaah Ametoa hukumu kali kwa kosa wizi. Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema, "Mkono wa mwizi unapaswa kukatwa hata kama kwa wizi wa robo dinaar" [Al-Bukhaariy Juzuu 8 Namba 781].

MTUME ANAKUTANA NA ALLAAH - JE, MTUME ALIPATA KUMWONA MOLA WAKE?

"Kisha akakaribia na akateremka. Akawa kama baina ya mipinde miwili au zaidi. Akamfunulia mja Wake, Alichomfunulia. Moyo haukusema uongo uliyoyaona. Je, Mnabishana naye kwa aliyoyaona? Na akamwona mara nyingine. Penye Mkunazi wa

Mwisho. Karibu yake ndipo ipo Bustani inayokaliwa. Kilipo ufuniko huo Mkunazi hicho kilichofunika. Jicho halikuhangaika wala halikuruka mpaka. Kwa yakini aliona katika Ishara kubwa kabisa za Mola wake. [Angalia Al-Bukhaariy Juzuu 9 Namba 609].

Waislamu wa mwanzo walitofautiana juu ya kwamba Mtume alimwona Mola wake kwa jicho lake au hapana. Mama wa Waumini ''Aaishah, Abu Hurayrah na Ibn Mas'uud (رضي الله عنهم) wanakataa kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwona Allaah kwa macho yake. Kuna riwaya kupitia kwa Ibn Abi Haatim kwamba Ibn Mas'uud alieleza Aayah zilizotajwa hapo juu, kwamba, "Mtume alimuona Jibriyl katika umbo lake halisi mara mbili. Na Mara Jibriyl alipokuwa katika umbo lake halisi basi alifunika anga yote kwa mwili wake. Kwa mara ya pili Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipomwona katika umbo lake halisi ni wakati wa safari yao ya kwenda Mbinguni. Na hiyo ndiyo maana ya maneno, "Naye Yuko juu kabisa ya upeo wa macho" (Tafsiyr Ibn Kathiyr) Hivyo aya hii inaonesha kuwa Jibriyl (عليه السلام) alijongea na kuwa karibu na Mtume (صلى الله عليه وسلم) (Fat-hul-Baariy ukurasa 263, 264 ya Juzuu 17). Amesimulia Masruuq (رضي الله عنه), "Nilimwuliza mama wa Waumini 'Aaishah (Radhiya Allaahu 'anha) "Ewe mama wa Waumini, Je Mtume alipata kumwona Mola wake?, mama wa Waumini 'Aaishah (رضي الله عنها) akasema, "Hicho ulichokisema kinafanya mwili wangu kusisimka na nywele kujivuta. Jua kuwa iwapo mtu atakwambia kitu katika hivi vitatu vifuatavyo ni mwongo: "Mtu akikwambia kuwa Muhammad (صلى الله عليه وسلم) alimwona Mola wake, ni mwongo huyo" Na kisha mama wa Waumini 'Aaishah (رضي الله عنها) akasoma aya, "Macho hayamfikilii bali Yeye Anayafikilia macho. Naye ni Mjuzi, Mwenye khabari," (Al-An'aam 6:103) "Na haikuwa kwa mwanadamu kwamba AllaahAmsemeze ila kwa wahyu (ufunuo) au kwa nyuma ya pazia." [Ash-Shuura 42:51]. Jambo la pili kama mtu atakwambia nini kitatokea kesho, ni mwongo" na Kisha akasoma Aayah, "…Na haijui nafsi yo yote nini itachuma kesho…" [Luqman 31:34] na pia akaongezea jambo la tatu kwa kusema, "Ye yote atakayekuambia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alificha baadhi ya wahyu alioletewa na Allaahkutangaza, ni mwongo na akasoma aya, "Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi…" [Al-Maaidah 5:67]. Kisha mama wa Waumini 'Aaishah (رضي الله عنها) aliendelea kusema, Lakini Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwona Jibriyl (عليه السلام) katika umbo lake halisi mara mbili. [Al-Bukhaariy Juzuu 6 Namba 378].

Kwa upande mwingine Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) alisema kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimuona Mwenyezi Mungu, na akasema kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwoma Mola wake mara mbili. [Tafsiyr Ibn Kathiyr]. Al-Haafidh, Ibn Hajr alisema, "Maelezo ya Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) yamekuja katika hali ya kutodhibitiwa (hayaelezi kama Mtume alimuona Mola wake kwa macho yake au vipi) wakati kauli za mama wa Waumini 'Aaishah (رضي الله عنها) na wenziwe zimedhibitiwa kwa kusema Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakumwona Allaah"Kwa macho yake". Tunaweza kuunganisha kauli hizo mbili kwa kusema mama wa Waumini 'Aishah (رضي الله عنها) alikataa mwono "Kwa macho yake" na kauli ya Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) kuwa ni kamuona kiroho". [Fat-hul-Baariy 8/608] Pili, kauli hizo mbili, ya mama wa Waumini 'Aaishah (رضي الله عنها) na ya Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما), kwa njia nyingine kuwa kauli ya Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) alisema kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimuona Mola wake wakati akiwa katika usingizi, jambo ambalo ni ndoto ya kweli na isiyokuwa alimwona Siku ya Mi'iraaj wakati kauli ya mama wa Waumini 'Aaishah (رضي الله عنها) inakataa kuwa Mtume hakumuona Mola wake wakati yeye akiwa macho, lakini kauli hiyo haikatazi kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwona Mola wake akiwa usingizini. Alichokana hapa ni kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakumuona Allaah (سبحانه وتعالى) kwa macho yake meupe, akiwa macho. Wale ambao wanao msimamo kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwona Mola wake kwa macho yake meupe wanaleta HadeethDhaifu. Hakuna HadeethSahihi ambayo inaeleza ya kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwona Mola wake kwa macho yake akiwa macho. Wenye msimamo huo wanaleta Hadeethya At-Tirmidhiy ambayo Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) anasema kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwona Mola wake. Ikrimah alimuuliza: "Vipi Aayah ambayo inasema, "Macho hayamfikilii bali Yeye anayafikilia macho.". Alijibu, kuwa ni wakati tu Allaahamezungukwa na Nuru, lakini Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwona Mola wake mara mbili. "Hadeethhii ni dhaifu" Kwa hali hiyo kwa namna jinsi ilivyo hakuna mgongano wa kauli na AllaahAnajua zaidi. [Sharh ya Uswuul Al-I'itiqaad cha Lailakiy, 93/512, As-Sunnah 1/181 na Swifat Al-Maqdisiy ukurasa 109 -111]

Zawadi Ya Mi'iraaj

'Abdullaah bin Mas'uud alisema, "RasuluLlaah alipewa vitu vitatu: alipewa Swalah tano, alipewa aya ya kumalizia Surah ya Al-Baqarah na kusamehewa kwa madhambi ya wale watu ambao hawamshirikishi Allaahmiongoni mwa umati wake." [Muslim Namba 329] Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "Allaah Alinipa ufunuo na Akasema kuwa Ummah wangu wanawajibika kuswali Swalah 50 kila siku; usiku na mchana. Nilishuka kwenda kwenye Mbingu ya Musa (عليه السلام) akaniluza, "Lipi Mola wako Amekupatia kwa ajili ya umati wako?, Nikasema, "Swalah Khamsini" Akasema Rejea kwa Mola wako na omba Akupunguzie katika idadi hiyo ya Swalah, maana watu wako hawawezi kubeba mzigo huo mzito. Kama vile nilivyotiwa katika mtihani na Wana wa Israeli, na nikawajaribu nikawaona kuwa walikuwa dhaifu sana na hawawezi kubeba mzigo kama huo." Hivyo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimgeukia Jibriyl (عليه السلام) kama vile akitaka kupata ushauri wake juu ya hilo. Jibriyl (عليه السلام) akasema, "Ndiyo, sawa, kama unataka hivyo". Na wakarejea tena juu kwa Mwenyezi Mungu." [Al-Bukhaariy Juzuu 9 Namba 608]

Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema, "Nilirejea kwa Mola wangu na kusema, "Ewe Mola wangu, Fanya vitu viwe vyepesi kwa ajili ya Ummah wangu. AllaahAlipunguza idadi ya Swalah 50 na kuwa tano kwa ajili yangu. Nilishuka chini nikaenda kwa Musa (عليه السلام) ambaye alisema, "Hakika watu wako hawataweza kubeba mzigo huu mzito. Rejea kwa Mola wako umwombe afanye wepesi wa hilo, Ewe Muhammad". Mimi nilijaribu kuwalingania Ummah wangu Wana Israeli ili wafanye kidogo zaidi ya hayo, lakini hawakuweza kuyafanya hayo bali waliishia kukata tamaa." [Al-Bukhaariy, Juzuu 9 Namba 608]. Basi nikawa natangatanga kati ya Mbingu ya Musa na kwa Mola wangu mwisho Allaah (سبحانه وتعالى) Akasema: "Kuna Swalah tano kila siku, usiku na mchana Ewe Muhammad. Kila Swalah imebeba uzito wa Swalah kumi, na hivyo hizo ni Khamsini vile vile. Mtu yeyote anayetia nia ya kufanya jambo zuri na asipolifanya basi atapata thawabu kwa hilo, na kama atalifanya hilo tendo, basi itaandikwa thawabu kumi kwa hilo. Wakati ambapo mtu aliyenuia kufanya

uovu na akaacha kuufanya haitasajiliwa hiyo na kama atafanya uovu huo basi utasajiliwa uovu mmoja tu. Hapo nikashuka kwa Musa (عليه السلام) na kumwambia hayo, Musa akasema," Nenda kwa Mola wako ili afanye mambo yawe mepesi zaidi". Juu ya kauli hiyo Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) akasema, "Nimekuwa nikienda kwa Mola wangu mara kwa mara hadi naona aibu kusimama mbele yake. (Muslim). Juu ya hilo Jibriyl ((عليه السلام akasema,"Kwa jina la Mwenyezi Mungu! Shuka sasa! Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaamka akiwa ndani ya Msikiti Mtukufu wa Makkah." (Swahiyh Al-Bukhaariy Juzuu 9 Namba 608) na pia ndani ya maelezo ya Al -Bukhaariy kuna maelezo zaidi kuwa, … Nilipoondoka nilisikia sauti "Nimetoa amri yangu na kisha nimewapunguzia uzito Waja Wangu".

Allaah (سبحانه وتعالى) Ameitukuza Swalah na kuipa daraja kubwa sana kwa kuifaradhisha katika usiku wa Mi'iraaj Amri zote zingine zililetwa na Jibriyl (عليه السلام) ardhini kwa Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم). Swalah ilifaradhishwa baada ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuitwa kwenda Mbinguni na mawasiliano yalikuwa ni moja kwa moja kutoka kwa Mola hadi kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Aya nyingi za Qur-aan na Hadeeth nyingi za Mtume (صلى الله عليه وسلم) zinashuhudilia utukufu na umuhimu wa Swalah.

Ibn Hajar anaandika katika sharh yake ya Al-Bukhaariy (1/460), "Hekima ya kufaradhishwa Swalah wakati wa Mi'iraaj ni kuwa hapo ndipo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipopata utukufu kamili kwa nje na ndani ya mwili wake. Alikoshwa kwa maji ya Zam Zam na kisha akanyunyuziwa na Iymaan na hekima. Kwa kuwa Swalah imetanguliwa na wudhuu, ilikuwa hasa mahali pake maamrisho ya Swalah yaletwe akiwa katika hali hiyo yaani baada ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kutakaswa na kusafishwa."

Allaah (سبحانه وتعالى) Anasema: "…Na Mkizihesabu neema za Allaahhamwezi kuzidhibiti," Kupunguzwa kwa idadi ya Swalah ni neema kutoka kwa Allaahna kisha Allaah Amesema: "Ni wachache katika waja wangu wanao shukuru." [Saba-a 34:13] na "Hakika mwanadamu ni mtovu wa fadhila kwa Mola Wake Mlezi" [Al-'Adiyaat 100:6]. Je, kuna neema gani tukufu ziaidi ya hii kuwa Swalah ambazo zilikuwa ni Khamsini zimepunguzwa na kuwa tano kwa siku, usiku na mchana na kisha malipo ya hizo Swalah tano ni sawa na Swalah Khamsini zile za mwanzo?

Ibn Hibbaan anasema katika Swahiyh yake (1/133): "Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) alifaradhishiwa Swalah Khamsini, amri hii ilikuwa ni mtihani mkubwa, mtihani ambao alitaka kumpima nao kipenzi Wake Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم). Wakati akimwambia kuwa Ummah wake wakaswali Swalah Khamsini alikuwa anajua fika kuwa wataswali Swalah tano tu na amri ya kuswali Swalah Khamsini ilikuwa ni mtihani tu! Hii ni sawa na maneno yetu kuwa Allaah (سبحانه وتعالى)

Anaweza Akaamrisha kitu kwa mja Wake ambaye atapokea amri hiyo lakini si lazima aitekeleze kwa vitendo. Mfano mzuri wa hilo ni pale Allaah (سبحانه وتعالى). Alipomwamuru Ibraahiym (عليه السلام) kumchinja mwanae mpenzi. Utashi wa Allaah (سبحانه وتعالى) kwa amri hii ilikuwa ni kuwa Amri Yake ipokelewe na ikubaliwe kikamilifu. Na pindi wote mzazi na mtoto waliposalimu amri na kujisalimisha kwa Mola wao, Allaah (سبحانه وتعالى). Alitoa kafara ya mtoto huyo badala yake kwa kafara kubwa sana. Kama Allaah (سبحانه وتعالى) Angelikuwa Anataka yatekelezwe yale aliyoyaamuru basi Ibraahiym angelikuta mtoto wake kachinjwa kweli. Hali kadhalika kutoa amri ya kuswali Swalah Khamsini kwa kila siku ilikuwa ni amri ya kukubaliwa lakini kitu kingine ambacho ni chepesi kwa matendo chenye uzito sawa sawa ndiyo kifanyike ambazo ni Swalah tano".

Yeyote anayedharau Swalah, siyo kwamba kakataa nguzo ya Uislamu bali pia kakataa zawadi kutoka kwa Allaah (سبحانه وتعالى). Swalah ni nguzo ya kwanza katika mpangilio aliowekewa binadamu na ndio ibada ya kwanza kuulizwa mja siku ya Qiyaamah na pia ilikuwa ni amri ya mwisho ambayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiitamka mpaka mwisho. Wakati Mtume (صلى الله عليه وسلم) akiwa katika maradhi yake ya mwisho alikuwa akisema: Swalah, Swalah na vile ambavyo mikono yenu ya kuume inavimiliki. [HadeethSwahiyh imesahihishwa na Imaam Al-Albaaniy, Ibn Maajah na Musnad ya Ahmad]. Mtu anapokufa hasemi ila maneno yale ambayo anayaona kuwa ni ya muhimu sana kwake na anapendelea watu wachukue ushauri wake wa mwisho. Hivyo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alituamuru kwa maneno hayo ambayo aliyaona kuwa ni ya muhimu sana "Tuchunge Swalah".

'Abdullaah bin Qart alisema kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "Tendo la kwanza ambalo mja atawajibika nalo siku ya Qiyaamah ni Swalah. Kama Swalah yake itakuwa ni nzuri basi matendo mengine yote yatakuwa ni mazuri. Na kama Swalah itakuwa ni mbaya basi matendo mengine nayo yatakuwa ni mabovu." [At-Twabaraaniy]

Alisema Abu Buraydah bn Al-Haasib: "RasuluLlaah amesema: "Kitu ambacho kinatutofautisha Waumini na makafiri na wanafiki ni jinsi tulivyo karibu na Swalah. Mtu asiyeswali anaangukia katika kundi la maka firi." [At-Tirmidhiy Namba 1083]

Allaah (سبحانه وتعالى) Anasema kuwa watu wa motoni watatupwa katika Jahanamu na wataulizwa: Kitu gani kimekusababisheni kuingia katika Moto wa Jahanamu? Nao watajibu, "Hatukuwa miongoni mwa wale waliokuwa wakiswali." [Al-Mudathir 74:42-43]. Hivyo jambo la kwanza ambalo wataungama itakuwa 'walikuwa wameacha Swalah'.

Umuhimu wa Swalah unaonekana katika Msikiti wa Qubaa. Msikiti huu ulijengwa wakati Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipohama kutoka Makkah kwenda Madiynah. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikaa sehemu za Qubaa siku nne kabla hajaingia mjini Madiynah, hakupanga kukaa Qubaa wala hakujenga chochote hapa. Kitu alichofanya hapa alijenga msikiti wa Qubaa. Kitendo cha Mtume (صلى الله عليه وسلم) kujenga msikiti hapa Qubaa kinaonesha umuhimu wa Msikiti katika Uislamu. Hivyo basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipeleka kikundi cha Maswahaba kwenda kupigana Jihaad. Aliwaambia waahirishe vita hivyo, waache kila kitu wakisubiri adhana. Anasema Anas bin Maalik (رضي الله عنه), "Daima mtu alipotoka nasi kwenda kupigana Jihaad dhidi ya watu wowote wale, hakuturuhusu kupigana hadi asubuhi na atasubiri kusikiliza kama kutatokea adhana. Akisikia adhana basi ataahirisha vita hivyo na kama hakusikia adhana basi aliamuru vita hivyo viendelee…" [Al-Bukhaariy Juzuu 1 Namba 584]

Ndugu Waislam, tusome tukio hili kwa mazingatio makubwa kwa kuyafanyia kazi mafunzo yanayopatikana ndani yake, na si kwa kukisherehekea, kufunga na kutenga siku maalum ya kula, kuswali Swalah za aina fulani na du'aa za namna fulani, kugawa vyakula na kufanya mikusanyiko ya masimulizi ya kuburudisha kama ambavyo imekuwa ni ada kwa baadhi ya watu, hayo yote hayajathibiti wala kufanywa na wema waliopita. Tuige matendo ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na watangu wema na tutafanikiwa insha-Allaah.